

“HCF” MLEZI WA KILA MTU USHUHUDA WANGU

Awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa yote aliyonitendea katika maisha yangu. Kama anavyojiuliza mwimba Zaburi, nami najiuliza nimrudishie nini Mungu kwa yote aliyonitendea? Yeye ni mwamba wa wokovu wangu, na sehemu yangu milele. Zaburi; 116:12, 73:25-26).

Kwa mara ya kwanza habari za ushirika wa kikristo katika huduma ya afya nilizisikia tangu mwaka 1972, wakati ambapo nilikuwa mwanafunzi wa mwaka wa pili pale chuo cha uuguzi Bugando, Mwanza. Kwa kupitia Ushirika huu ndipo nilikata shauri na kuokoka. Namshukuru Mungu sana mimi na rafiki yangu Magdalena tulishirikishwa na Daktari Samuel Nkulila kuhusu faragha ya walokole (Tukutendeleza) iliyokuwa inafanyika mjini Mwanza. Kikundi hicho wengi wao walikuwa watu wazima isipokuwa sisi wawili tu. Nawashukuru sana walitulea vyema.

Mwaka 1975, nilimaliza masomo yangu na kuanza kazi KCMC Moshi. Hakukuwa na tawi, bali binafsi niliendelea kushuhudia wagonjwa na kuwaombea. Pia nilipoenda Moshi yeye aliyenishudia kwa mara ya kwanza Dr. Samwel Nkulila alijulisha kwa wandugu waliokuwa huko na walinilea vizuri sana, Nilijiunga na faragha za waliookoka na vikundi vya ushudiaji na uimbaji. (Waebrania 13:7-8).

Mwaka 1978 nilijiunga na mafunzo ya ualimu wa uuguzi Dar es Salaam, baada ya kumaliza nilipangiwa chuo cha Uuguzi Bugando na baada ya kuolewa nikarudi Muhimbili. Nikiwa pale Muhimbili ndipo nilijihusisha tena baada ya kukutana na wenzangu wengi waliokuwa na ufahamu wa ushirika huo. Nakumbuka mmoja wao alikuwa Mama E. Mushi, ambaye alikuwa ni Muuguzi mkuu pale Muhimbili pamoja na makamu wake Mama Grace Gumbo walinipokea vizuri sana.

Jambo hili ninalifananisha na punje (punje ya haradali) iliyotupwa ndani mwangu 1972, ambayo ilikua taratibu na baadaye kuja kuibuka kwa nguvu mwaka ule wa 1987 (Luka 13:19) tulipokwenda kwenye kongamano la ‘All Africa Jubilee’ kule Nakuru Kenya.

Baada ya Kongamano hilo, tulirudi Dar es Salaam na dada Sue Willan muuguzi aliyekuwa anafanya kazi hospitali ya Mvumi, aliombwa na makao makuu ya ‘HCFI’

awe mtumishi wa kudumu hapa petu Tanzania. Hivyo basi, mnamo mwaka 1987, UKHA Tanzania ilianza shughuli zake rasmi kama idara maalumu chini ya usimamizi wa Umoja wa Kujisomea Biblia (UKB) Tanzania.

Kamati ya taifa (NAT) ilianzishwa kwa mara ya kwanza mwaka huo, nikawa katibu 1987 -2000, pia M/kiti 2001 -2007, Namshukuru Mungu niliweza kutumika kwa namna hiyo.

Mwisho

- Namshukuru Mungu kupitia makongamano nilipata kuulewa Ushirika huu wa Kikristo katika huduma ya Afya vizuri.
- Niliweza kujifunza kutoka kwa wengine, Kwa mfano nakumbuka baada ya kuhudhuria kongamano kule Limuru Kenya lilitutia ujasiri wa kuanza kamati na kuendesha shughuli zetu (NAT). Baada ya kuhudhuria kongamano la kwanza la kimataifa, Exeter Uingereza, mwaka 1990 tuliporudi nasi tulipanga kongamano letu la kwanza nchini mwaka 1992, kule Jeshi la Wokovu, Dar es Salaam.
- Kwangu Mimi makongamano yamekuwa kichocheo (uamsho) kikubwa katika huduma hii kila nilipohudhuria nilipata nguvu mpya ya kuendelea mbele na nipo kwenye kamati miaka yote hii, hadi sasa.
- Kufuatana na niliyoyataja hapo juu kwa kujihusisha na HCF, imenilea katika maeneo mbalimbali ya kiroho, kiutawala pamoja na niliyoyataja hapo juu. Jina la Bwana libarikiwe.

Imeandaliwa na: Mrs. Margareth Philemon